



Ikiwa ulikagua jedwali/boksi yoyote, muulize daktari wa mtoto wako kuhusu kipimo cha damu yake.

Kama mtoto wako ni mdogo kuliko miaka 6, kagua yote ambao ni kweli kwenye orodha hii.

- Mahali ninapoishi palijengwa kabla ya 1950.
- Mahali ninapoishi palijengwa kabla ya 1978, na pamekuwa na matengenezo, kumepakwa rangi au mikarabati imefanyika hivi karibuni.
- Mtu anayeishi na mimi huenda hutumia risasi/lead kazini. Mifano: wapakaa rangi, makandarasi, wachakataji wa chuma/metali.
- Mtoto wangu ana kaka, dada au jirani ambaye alikuwa na sumu ya risasi[lead].
- Mtoto wangu au mimi tulizaliwa katika nchi nyingine.
- Mtoto wangu anaweka vitu vingi visivyo chakula kinywani mwake.

Nini kibaya kuhusu risasi/lead?

Risasi/Lead huweza kusababisha:

- Ulemavu wa majifunzo
- Matatizo ya Tabia
- Upungufu wa akili
- Uharibifu wa kusikia
- Uchelewaji wa lugha au usemi

Jinsi gani sumu ya risasi/lead hutokea?

Vumbi kutoka kwa rangi ya risasi[lead] katika nyumba za zamani karibu kila mara husababisha sumu ya risasi/lead.

Vumbi ya risasi hukusanyika kwenye sakafu na katika maeneo ambapo watoto wanatia mikono yao na kuchezea na vinyago/midoli. Watoto, hasa wale walio chini ya umri wa miaka 3, mara nyingi huweka mikono yao na vinyago katika vinywa vyao. Hili hufanya iwe rahisi kwa vumbi ya risasi/lead kuingia na kuharibu miili ambayo bado inakua.

Nitajuaje kama mtoto wangu ana sumu ya risasi [lead]?

Njia pekee ya kujua ni ya kupima damu. Watoto wengi walio na sumu ya risasi/lead hawaonekani wala hawajishike kama wagonjwa.

Vipi ikiwa mtoto wangu anayo MaineCare?

MaineCare inaomba kipimo cha damu kwa ajili ya risasi [lead] wakati watoto wana umri katika miaka 1- na 2.

Unaweza kumuuliza daktari wa mtoto wako kwa ajili ya kipimo cha risasi/lead.

Geuza kwa ajili ya njia za kulinda mtoto wako salama dhidi ya risasi/lead. →

Linda Familia Yako.

Kagua mtandao huu: maine.gov/healthyhomes

• Ita kwa ajiri ya ushauri: **866-292-3474** • TTY: **Ita Maine Relay 711**

Sumu ya risasi/lead

Nawezaje kumlinda mtoto wangu salama?

Lead Tipsheet #10



January 2019

Kama ulikagua jedwali/boksi zozote kwenye upande mwingine wa karatasi hii, hapa ni baadhi ya vidokezo kwa ajili ya kuweka watoto wako mbali na lead/risasi.

Angalia Rangi Katika Nyumba Yako

- ✓ Angalia madirisha yaliyopakwa rangi, milango, na sakafu kwa kumenyeka, mimenyo au vibanzi vya rangi. Weka watoto mbali na maeneo haya.
- ✓ Mwaambie mwenye nyumba kuhusu rangi iliyoharibika.



Weka Vitu Safi

- ✓ Safisha sakafu, zunguko za madirisha na juu ya meza ukitumia matambara ya kuosha mara moja kwa wiki.
- ✓ Osha mikono ya mtoto wako kabla ya kukula au kulala.
- ✓ Safisha vinyago mara moja kwa wiki na kuweka vinyago mbali na maeneo yaliyo na vibanzi vya rangi.

Chakula, Machupa, Nyonyo Bandia

- ✓ Lisha mtoto wako mezani au katika kiti kilicho juu.
- ✓ Usimruhusu mtoto wako kula chakula kilichoanguka kwenye sakafu.
- ✓ Osha nyonyo bandia na machupa vinapoangukia kwenye sakafu kabla ya kumpatia mtoto wako.



Miradi ya Upakaaji wa Rangi au Ukarabati wa Nyumba

- ✓ Jifunze jinsi ya kudhibiti vumbi ya risasi/lead kabla ya kuanza miradi yoyote ya ukarabati au upakaaji wa rangi kwenye nyumba.
- ✓ Pima kwa ajili ya vumbi ya risasi/lead baada ya kumaliza mradi. Omba vyombo vya kupima bila malipo kwa : maine.gov/healthyhomes.
- ✓ Ajiri mkandarasi aliyethibitishwa na EPA RRP” kufanya kazi hiyo. Jifunze zaidi kwenye epa.gov/lead.

Usilete Risasi/Lead Kutoka Kazi Yako

- ✓ Kama unatumika na risasi/lead katika kazi yako, badilisha viatu na nguo zako mara moja/hapo. Weka nguo chafu katika mfuko wao pekee au ya zuwia. Fua nguo za kazi pekee mbali na mavazi za familia.
- ✓ Oga mwili wote kabla ya kugusa mtoto wako.

Linda Familia Yako.

Kagua mtandao huu: maine.gov/healthyhomes

• Ita kwa ajiri ya ushauri: **866-292-3474** • TTY: **Ita Maine Relay 711**

